

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

12 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 12 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

234. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED
KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Wakazi wa Liwale waliathirika na vurugu za Uchaguzi wa Mwaka 2020 na mali za Wananchi na Serikali zilichomwa moto:-

Je, Serikali kupitia Mfuko wa Maafa ina mpango gani wa kuwafuta machozi Wananchi walioathirika na vurugu hizo.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

235. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Makanya kwenda kwenye Machimbo ya Jasi Wilayani Same.

236. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini barabara za kutoka Rubanga, Isulwabutundwe, Mkoba, Kukuruma, Kamhanga, Kishinda na Mkolani zitatengewa fedha na TARURA kwa ajili ya kuanza ujenzi.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**237. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL
MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Bulamba – Bukonyo hadi Masonga yenye urefu wa Km 32.23 kwa kiwango cha lami.

**238. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA
KANDEGE (KALAMBO)**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, mpango wa Serikali wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege eneo la Kisumba Wilayani Kalambo umefikia hatua gani kwa sasa.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA
YA HABARI:**

**239. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano ya simu kwenye Vijiji vya Igalula ambavyo havina mawasiliano ya simu.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

240. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itafuta Hati ya Mashamba yaliyotelekezwa kwa zaidi ya miaka 20 Wilayani Mkinga hususan Shamba la Kwamtili ili ardhi hiyo igawiwe kwa Wananchi.



WIZARA YA MAJI:

241. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza changamoto ya maji katika Wilaya ya Nkasi.

242. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

(a) Je, ni lini Serikali itaimarisha na kuboresha miundombinu ya maji ya Mamlaka ya Maji Makonde ili Wananchi waweze kupata maji ya uhakika;

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kuboresha upatikanaji wa maji Newala Vijijini ambapo kwa sasa uzalishaji ni ujazo wa lita 6,700 kwa siku badala ya lita 23,741.

IV. UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE:

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
12 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**